


# Kupambana ili Kuishi

**Watoto wanaoishi wenyewe mitaani nchini Tanzania na Kenya**

Muhtasari

We fight for children living on the streets

RAILWAY children

Fighting for street children

# Kupambana ili Kuishi:

## Watoto wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya

Muhtasari

Railway Children

# Kupambana ili Kuishi: Watoto wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya

## Muhtasari

Muhtasari huu unaangazia matokeo na mapendekezo yatokanayo na mradi wa utafiti uliofadhiliwa na Railway Children.

Dhana na muundo wa utafiti, kazi ya utafiti wenyewe, uchambuzi wa takwimu na uandishi wa taarifa ulifanywa na Emilie Smeaton.

## Taarifa Zaidi

Kwa maelezo zaidi kuhusiana na utafiti huu tafadhali wasilianana na:

Pete Kent
Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki
Railway Children
1 The Commons
Sandbach
Cheshire
CW11 1RG

Tel: (01270) 757596

Barua pepe: pete.kent@railwaychildren.org.uk

Anna Thor, Programme Development Officer
Railway Children Africa
P.O. Box 138
Mwanza
Tanzania

TZ: +255 (0) 685 22 74 84

Barua pepe: anna.thor@railwaychildren.org.uk

Kampuni : 77698

NGO Compliance No: 1381

Habari kuhusu Railway Children zinaweza kupatikana katika tovuti: www.railwaychildren.org.uk

Ili kupata nakala kamili ya taarifa ya utafiti huu, tafadhali wasiliana na Railway Children.

Registered Charity No. 1058991

ISBN Number:
978-0-9563998-3-0

Ripoti hii ya utafiti inawekwa rasmi kwa ajili ya kumbukumbu ya Rweyemamu Silasi, aliyejulikana zaidi kama Ustadhi. Ustadhi aliuawa kikatili na kundi la watu katika mitaa ya Jiji la Mwanza, Kaskazini mwa Tanzania tarehe 5 Agosti, 2011 baada ya kutuhumiwa kuwa ameiba simu ya kiganjani. Ustadhi alikuwa akiishi mitaani kwa zaidi ya miaka minne lakini alishaanza kujijengea maisha yake mbali na maisha ya mitaani; alishaacha kuvuta/kunusa gundi, alishaanza biashara ndogondogo na alikuwa amekodi chumba kidogo yeye na rafiki zake. Kifo cha Ustadhi hakikutangazwa katika vyombo vya habari na hakuna mtu yeyote aliyekamatwa au kushtakiwa kufuatia kifo chake. Ustadhi alikuwa na umri wa miaka 17.

## Utangulizi

Popote walipo duniani, watoto wanaoishi wenyewe mitaani wanafanya hivyo kwa sababu wana uchaguzi mdogo sana tofauti na huo. Wengi wanalazimika kukimbia nyumbani; wengi zaidi wanachagua kuishi mitaani kwa kuwa nyumbani pamegeuka chungu cha moto wa ukatili kisichoweza kuvumilika, kutelekezwa na kudharauliwa. Kwa bahati mbaya, mara nyingi pia, mambo haya haya ndiyo wanayotendewa watoto hawa wawapo mitaani.

Watu wengi hawatambui uwepo wa watoto hawa, au wanawaona kama wasumbufu tu ambao kwa sababu fulani wanapendelea kuishi mitaani. Watoto wenyewe wanaonekana kama ‘tatizo’ badala ya jamii ambayo imewakosea na imeshindwa kukidhi mahitaji yao. Watu wengi huwa hawawaoni watoto hawa; wachache zaidi wanawasikiliza. Railway Children tunawaona vizuri sana watoto hawa na tunaamini kuwa ni wajibu wetu kuwapa sauti ambayo si tu kwamba jamii itaisikia lakini itaanza kuisikiliza.

Railway children imekuwa ikifanya kazi kwa ubia na mashirika yaliyopo nchini Kenya na Tanzania tangu mwaka 2006. Kazi inayofanywa na mashirika haya inastahili kupongezwa sana. Watoto na vijana wengi waliokuwa wanaishi mitaani katika maeneo haya kwa sasa wana mahusiano mazuri ya kifamilia, wanahudhuria shule au wanaweza kujitegemea wenyewe kiuchumi kutokana na kazi zao. Bila msaada wa mashirika haya, watoto hawa wangeendelea kuishi mitaani wakihangaika katika maisha ya kikatili, yanayoambatana na matumizi ya dawa za kulevya pamoja na kunyanyaswa kijinsia.

Mashirika haya hayapo peke yao katika kutambua mahitaji ya watoto waliopo mitaani. Watu wengi binafsi huonyesha ukarimu kwa watoto wanaoishi mitaani. Serikali kuu na serikali za mitaa nchini Kenya na Tanzania zinatambua mahitaji ya watoto waishio mitaani na zimefanya jitihada kubwa kufanya kile kinachowezekana ili kuwasaidia watoto moja kwa moja au kwa ushirikiano na mashirika ya kijamii.

Hata hivyo, imeonekana wazi kwetu tangu tulipoanza kufanya kazi katika eneo hili kwamba kuna idadi kubwa ya watoto wanaoishi mitaani ambao hubakia huko huko licha ya huduma kadhaa ambazo hutolewa kwa juhudi kubwa na serikali na mashirika ya kijamii. Tunahitaji kufahamu kwa undani na kwa usahihi zaidi sababu ya hali hii.

Watoto wote walioshiriki katika utafiti walishakaa angalau kwa wiki nne mitaani; baadhi walishaishi mitaani kwa miaka kadhaa. Tunataka kuwapatia watoto hawa sauti, watoto ambao ni vigumu sana kuwafikia, watoto ambao wamekumbana na matukio ya kutisha na kutia simanzi.

Hii inaweza kumaanisha kuwa hawa ni watoto ambao wana matatizo na tabia mchanganyiko zisizo za kawaida katika jamii: hawa ndio watoto ambao sisi tunaamini wanahitaji zaidi msaada wetu.

Utafiti huu ni jaribio la kuwapatia sauti hiyo baadhi ya hawa watoto; kuwapatia fursa ya kutoa masimulizi yao ili tuweze kujifunza kutoka kwao. Matokeo ya utafiti huu yataisaidia Railway Children kurekebisha mipango yetu ya sasa na pale inapobidi kuandaa mipango mipya itakayomudu vema zaidi kukidhi mahitaji ya watoto hawa. Tunatumaini kuwa wewe, msomaji, kwa nafasi yoyote unayoweza, utarekebisha mipango yako, sera au labda tabia yako tu, ili kuelewa vema zaidi na kuhudumia mahitaji ya hawa watoto.

Ningependa kurudia kuwa: makusudi ya utafiti huu ni kupata uelewa zaidi juu ya maisha ya watoto ambao ni vigumu sana kuwafikia. Hii haimaanishi kuwa watoto wote waliokimbia kutoka nyumbani wanawakilishwa katika utafiti huu kwa kuwa utafiti unalenga wale ambao tayari wamefanikiwa kufika katika vituo vya huduma vilivyopo. Wananchi wa Kenya na Tanzania wanapaswa kujivunia ukweli kwamba watoto wengi wanaishi katika mazingira magumu sana lakini hawakimbilii mitaani kwa sababu ya msaada unaotolewa na familia pana, ukoo, majirani na mashirika ya kijamii.

Nilipata bahati ya kufanya mahojiano machache na watoto nchini Tanzania kama sehemu ya utafiti huu. Napenda kuwashukuru watoto wote walioshiriki katika utafiti kwa ujasiri walionao wanaposimulia habari zao. Wote tuliguswa sana na jinsi walivyokuwa na shauku ya kutaka wengine wafahamu habari zao ili kwamba watoto wenzao watakaojikuta wanaishi mitaani siku zijazo watendewe kwa heshima na utu zaidi. Napenda pia kuwashukuru wabia wa Railway Children kwa uelewa wao, uvumilivu na muda mwingi waliotupatia ili kufanya utafiti huu. Shukrani pia kwa mtafiti mkuu na mwandishi, ambaye kujitoa kwake kuhakikisha ustawi wa kila mtoto aliyehusika kunatugusa na kututia moyo sisi wote. Na mwisho, asante kwako wewe msomaji, kwa kutumia muda wako kusoma taarifa hii.

**Pete Kent**

Mkurugenzi wa Kanda ya Afrika Mashariki

Railway Children

## Yaliyomo


| | |
|---|---|
| Utangulizi | 1 |
| Sera na Utekelezaji | 2 |
| Njia za utafiti | 2 |
| Maisha kabla ya kuja mitaani: Familia na Nyumbani | 3 |
| Uzoefu wa kuishi pekee mitaani | 4 |
| Uzoefu wa Watoto na Vijana kuhusu Mashirika yanayowahudumia | 7 |
| Mahusiano, utambulisho na Ustahimilivu | 8 |
| Maoni ya kuhitimisha | 8 |
| Hatua muhimu kwa ajili ya Sera, Utekelezaji na Utafiti | 9 |

## Utangulizi

### Reuben

Reuben ni mtoto mwenye umri wa miaka 11 ambaye mwonekano wake ni wa mtoto wa umri mdogo zaidi. Wazazi wa Reuben walifariki alipokuwa mdogo na alilelewa na kaka yake mkubwa. Kaka yake aliamua kutoroka nyumbani na kwa kukosa mtu wa kumpatia maji na sabuni ya kuogea na chakula, Reuben alifikiri kuwa atakufa iwapo ataendelea kukaa hapo nyumbani. Alishasimuliwa mambo mazuri kuhusu mjini na alifikiri kuwa kulala nje mitaani itakuwa bora zaidi kuliko kukaa nyumbani na kwamba Yesu atamlinda. Reuben alikuwa na imani kwamba Msamaria Mwema atamruhusu kukaa na kuishi naye kwake, kumpeleka shule na kumsaidia kupata kazi nzuri atakapomaliza shule. Halafu, atakapokuwa anafanya kazi nzuri, atamtunza huyo Msamaria Mwema aliyemsaidia kuondoka katika maisha ya kuishi mitaani.

Reuben alikuwa akiishi katika banda bovu pamoja na wavulana wengine wadogo lakini baada ya kuona vitendo vya ngono kati ya baadhi ya wavulana, jambo ambalo lilimhuzunisha na kumnyima utulivu, aliamua kuachana na maisha yaliyoonekana salama kiasi kwenye banda hilo na kuamua kuanza kulala mitaani.

Baada ya miezi miwili hivi mitaani, Reuben alifikiri kuwa maisha ya mitaani siyo mazuri kwa sababu mtu anaweza kumchukua na kumwuza, kumdhalilisha kwa namna mbalimbali au kumwua. Reuben anafikiri kwamba maisha yake yapo hatarini mara zote, hasa wakati anapolala nje na anaogopa kuwa mtu anaweza kuja na kumwua. Reuben anasimulia namna watoto wengine wanaoishi peke yao mitaani wamekuwa wakipanga mbinu za kumwibia koti lake kwa kumshambulia kwa kutumia bisibisi.

Msaada pekee anaoupata Reuben ni kutoka kwa kina mama wachache ambao humpa mabaki ya chakula baada ya kwenda kuwatekea maji, na watu wachache wanaompa msaada anapowaomba. Anatamani kusaidiwa lakini anafahamu kuwa mtu anaweza kukuambia atakusaidia lakini kinyume chake akakudhuru. Reuben anatamani apate mtu wa kukaa naye na kupata chakula, kuwa na kitanda cha kulalia na kupelekwa shule. Hili, Reuben anaamini, litamfanya aonje maisha mazuri. Reuben hafikirii habari ya siku nyingi zijazo kwa sababu hana hata hakika ya kesho: labda Mungu atamchukua na hataishi kuiona siku nyingine.

Reuben anafikiri kuwa ni vema watu wawasaidie watoto wa mitaani kwa namna ye yote wanayoweza kwa kuwapatia malazi na chakula, kuwapeleka shule na kuwapatia mavazi. Kisha, watoto hawa wakikua na kupata kazi watawasaidia hao waliowasaidia.

- Taarifa hii ya utafiti inatokana na maisha halisi ya watoto wanaoishi katika mazingira hatarishi kabisa na waliotengwa: wale ambao wameishi wenyewe mitaani kwa kipindi kisichopungua wiki nne au zaidi nchini Tanzania na Kenya.
- Watoto walioshiriki katika utafiti huu wanaishi mitaani muda wote na hawarudi nyumbani usiku ili kuishi na familia zao au walezi wengine.
- Utafiti mwingi umeshafanyika sehemu mbalimbali duniani ukihusisha watoto na vijana waishio mitaani. Sauti za watoto wanaoishi mitaani zinakosekana katika tafiti mbalimbali zinazojielekeza kushughulikia suala la watoto wa mitaani na ushauri mbalimbali unaolenga kushughulikia mahitaji yao.[1] Kwa kuzingatia hilo, Railway Children iliamua kuweka mkakati wa kufanya utafiti nchini Tanzania na Kenya ili kukusanya takwimu hizo.[2] Matokeo ya utafiti huu yatasaidia katika upanuzi wa kazi za Railway Children katika nchi mbili hizi na kuendeleza mipango ya kazi inayolenga kukidhi mahitaji ya watoto wanaoishi wenyewe mitaani na kuwawezesha kuwa na maisha bora zaidi.
- Malengo ya utafiti yalikuwa ni kupata, kwa maneno ya watoto wenyewe, uzoefu wa maisha ya watoto wa Tanzania na Kenya, wenye umri chini ya miaka 16, wanaoishi peke yao mitaani kwa zaidi ya wiki nne; kuwasilisha mtazamo na hali halisi ilivyo kwa sasa kuhusu nini maana ya kuishi peke yako na hasa katika mitaa nchini Tanzania na Kenya; kutoa ushahidi wa hakika unaoelezea maisha na uzoefu wa watoto waishio mitaani nchini Tanzania na Kenya; na kutambua sera zilizopo na mapendekezo ya nini cha kufanya ili kukidhi mahitaji ya watoto wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya.
- Shabaha ya utafiti ilikuwa kupata maoni na uzoefu wa watoto waliotengwa na ambao wapo katika hatari kubwa zaidi, mfano wale ambao hawajapata huduma zozote na hawajulikani kwa watoa huduma au wale wanaojulikana kwa watoa huduma, na wanaweza kuwa wamepata huduma wakati fulani, lakini mazingira na hali zao ni tete kiasi kwamba huduma zitolewazo kwa sasa hazijaweza kukidhi mahitaji yao.
- Yapo majukumu mbalimbali ambayo yametekelezwa na serikali ili kulinda na kutunza watoto katika nchi zote mbili, ikiwa ni pamoja na watoto wa mitaani. Hata hivyo, huduma zitolewazo kwa watoto wa mitaani kupitia taasisi za kiserikali hazitoshelezi kabisa.
- Watoto na vijana wapatao tisini na tatu (93) walishiriki katika utafiti huu uliofanyika katika sehemu mbili nchini Tanzania na sehemu mbili nchini Kenya, wengi wao wakikadiriwa kuwa na umri wa kati ya miaka 13 na 16. Kutokana na ukweli kuwa ilikuwa nadra kuwaona wasichana kwa urahisi mitaani, wasichana sita tu walishiriki katika utafiti huu. Majina ya watoto na vijana wote walioshiriki katika utafiti huu yamebadilishwa ili kulinda utambulisho wao na kuhakikisha kuwa hawafahamiki.
- Taarifa ya utafiti imewekwa katika vipengele ambavyo vipo katika maeneo yafuatayo:
  - maisha kabla ya kuja mitaani: familia na nyumbani
  - uzoefu wa kuishi pekee mitaani
  - uzoefu wa watoto na vijana juu ya taasisi zinazowahudumia
  - Mahusiano (attachment), Utambulisho (identity) na Ustahimilivu (resilience)

1 This has also been highlighted in a recent article: McAlpine K Henley R Mueller M & Vetter S (2009) 'A Survey of Street Children in Northern Tanzania: How Abuse or Support Factors May Influence Migration to the Street' Community Mental Health 46 pg 26 – 32.

2 Railway Children had previously commissioned research addressing the lives of children who spend time on the streets in the UK and the methodologies and learning from this project were used to inform the research in Tanzania and Kenya.

## Sera na Utekelezaji

- Tanzania na Kenya zimeridhia sheria za kimataifa na kujiwekea sera mbalimbali za ndani ya nchi na mikakati inayohusu haki za watoto. Miongoni mwa sera hizo zipo zinazohusiana moja kwa moja na watoto waishio mitaani.
- Tanzania na Kenya zimeridhia kutekeleza Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Mtoto (UNCRC). UNCRC ni chombo cha kisheria ambacho kinaelekeza na kinasisitiza haki za msingi za watoto duniani pote na hii inahusisha, haki ya kuishi; kujiendeleza/kuendelezwa kwa kadiri ya uwezo wa mtoto; kulindwa dhidi ya madhara na mazingira yanayoweza kumdhuru, kumnyanyasa na kutumiwa kwa njia ya kudhulumiwa; kushiriki kikamilifu katika maisha ya kifamilia, kitamaduni na kijamii.[3]
- Tanzania na Kenya kwa pamoja zimetia saini mkataba wa UNCRC na Makubaliano ya nchi za Kiafrika juu ya Haki na Ustawi wa Watoto (ACRWC).
- Kamati ya Haki za Watoto imeshauri kuwa serikali ya Tanzania: itayarishe mpango mkakati unaokidhi ili kushughulikia na kupunguza idadi ya watoto waishio mitaani; kuhakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya watoto wa mitaani yanatimizwa, ikiwa ni pamoja na lishe, malazi, huduma za afya na elimu; kupanua uelewa wa masuala ya watoto wa mitaani ili kubadili mtazamo hasi wa jamii kuhusu watoto wa mitaani, hasa miongoni mwa wasimamizi wa sheria; na kuhakikisha kuwa watoto wa mitaani wanapatiwa huduma ya kurejeshwa na kushirikishwa tena katika jamii.
- Kamati ya Haki za Watoto imetoa ushauri mbalimbali kwa serikali ya Kenya ikiwa ni pamoja na kwamba, inapaswa kuainisha na kushughulikia kiini au sababu ya watoto kuishi mitaani, kuandaa mikakati ili kupunguza idadi ya watoto waishio mitaani; kuhakikisha kuwa mahitaji ya msingi ya lishe, elimu, afya na ulinzi kwa watoto wa mitaani yanapatikana, kuamsha ufahamu wa tatizo na kupunguza kuwanyanyapaa watoto wa mitaani, hasa wasimamizi wa sheria; kuhakikisha kuwa watoto wa mitaani wanapatiwa huduma ya kurejeshwa na kushirikishwa tena katika jamii.[4]
- Sera na mipango mbalimbali ya kutoa msaada kwa watoto waishio mitaani imeshaandaliwa. Nchini Kenya, Sheria ya Watoto 2001 (kwa sasa inafanyiwa marekebisho) inayaweka maazimio ya UNCRC na Makubaliano ya nchi za Afrika juu ya Haki za Mtoto yaendane na mazingira ya nchi hiyo, hivyo kuwekea mkazo masuala ya haki na ustawi wa watoto na sheria juu ya masuala ya wajibu wa wazazi, mahakama za watoto, na usimamizi wa huduma kwa watoto. Nchini Tanzania Sheria ya Mtoto ya mwaka 2009 inajaribu kuliweka Azimio la Umoja wa Mataifa juu ya Haki za Mtoto[5] kwa kuingiza mabadiliko na kuunganisha pamoja sheria mbalimbali zinazohusiana na watoto; kufafanua haki za mtoto; kulenga kuhamasisha, kulinda, na kudumisha ustawi wa mtoto; kuweka misingi ya kisheria juu ya malezi ya kambo; kuasili watoto na uangalizi wa mtoto; vile vile kusimamia ajira na mafunzo ya ufundi na kuwa na vipengele vya kisheria vya kutosha kwa watoto walio katika mgongano na sheria.

## Njia za utafiti

- Uchunguzi wa awali ulifanyika ili kuamua njia zitakazotumika katika utafiti zikitilia maanani mwingiliano wa tamaduni na asili ya mtafiti mkuu aliyeongoza utafiti nchini Tanzania na Kenya ambaye ni mzungu kutoka Uingereza.
- Watafiti wote waliohoji watoto mitaani walikuwa na uwezo wa kuzungumza lugha mbili na waliweza kuwahoji watoto na vijana kwa Kiswahili, isipokuwa mtafiti mkuu na Mkurugenzi wa Railway Children katika kanda ya Afrika Mashariki, ambaye aliendesha utafiti akisaidiwa na mkalimani. Umakini mkubwa ulizingatiwa kuhakikisha kuwa tafsiri sahihi na ulinganifu wa maana ya kilichozungumzwa kinawasilishwa vilivyo kwa kutilia maanani utamaduni na lugha. Baada ya kuafikiana kuhusu usahihi wa mahojiano yaliyotafsiriwa ndipo uchambuzi ukafanyika. Inafaa kutambua, hata hivyo kuwa, pamoja na taratibu zote zilizofuatwa ili kupunguza athari za kutafsiri, maamuzi yanayochukuliwa kwa kuzingatia kazi iliyotafsiriwa yanaweza kuwa na athari kwenye utafiti.[6]
- Ili kufahamu kwa undani maisha ya watoto wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya, utafiti ulifanyika katika mazingira halisi ya wahusika ili kuona mahusiano na kazi zao katika mazingira wanayoishi.
- Wengi wa watoto na vijana walioshiriki katika utafiti huu walifikiwa huko huko mitaani, ambapo usaili/mahojiano yalifanyika. Watafiti wa mitaani walifanya mahojiano na watoto na vijana walioshiriki, wakiwa na mtaalamu ambaye anafahamika na vijana na watoto hao, ambaye aliwatambulisha watafiti kwa watoto mmoja mmoja au wakiwa kwenye kikundi. Baadhi ya watoto na vijana waliwaendea watafiti wakiomba washiriki katika utafiti. Wakati mwingine watoto na vijana hao walizungumza na watafiti zaidi ya mara moja.
- Juhudi zilifanyika ili kuhakikisha kuwa watoto na vijana ambao walikuwa hawafahamiki katika taasisi za kutoa huduma walishiriki katika utafiti, na pia kupata mtazamo wa watoto na vijana ambao wameishi katika vituo na kupata huduma mbalimbali zinazotolewa kwa watoto wa mitaani.
- Kutokana na uchache wa wasichana kuonekana mitaani, wasichana watatu ambao wanaishi katika kituo cha watoto waliweza kushiriki katika utafiti.
- Idadi ndogo ya vijana wenye umri zaidi ya miaka 16 walishiriki kwenye utafiti; hawa walikuwa na uzoefu wa kuishi mitaani kwa wiki nne au zaidi wakiwa chini ya miaka 16 lakini kwa sasa hawaishi tena mitaani. Hii iliwezesha kupata takwimu au taarifa ambazo zilitoa mwanga juu ya uzoefu na maoni ya vijana wenye umri mkubwa ambao waliishi mitaani kwa miaka kadhaa na kufikiri juu ya matokeo ya muda mrefu.
- “Grounded theory approach”[7] ilitumika kutayarisha nadharia nyingine ndogondogo ambazo zinajitosheleza kitakwimu na kuwakilisha kile kinachotokea katika ulimwengu halisia. Uchambuzi wa takwimu ulifanyika kwa ngazi mbili. Ngazi ya kwanza ilifanyika wakati wa kazi za mitaani. Ngazi ya pili ya uchambuzi ilifanyika kwa kutumia programu ya kompyuta inayoitwa “Atlas.ti” kutambua mada na masuala mbalimbali na kufanya ulinganifu na mahusiano yaliyopo katika takwimu zilizokusanywa.

3 www.unicef.org/crc/ 12th August 2010.
4 Committee on the Rights of the Child, 44th Session: Consideration of the reports submitted by state parties under Article 44 of the Convention. Concluding remarks: Kenya
5 Law of the Child Act 2009
6 Birbili M (2000) Translating from One Language to Another' Social Research Update Issue 31.
7 Glaser B & Strauss A (1967) The Discovery of Grounded Theory Chicago: Aldine.

- Umakini mkubwa ulizingatiwa kuhusu masuala ya maadili kijamii, kwa mfano kuhakikisha kuwa watoto na vijana walioshiriki walijulishwa kikamilifu juu ya utafiti, waliombwa kuthibitisha kuwa wanaridhia wenyewe kuhojiwa na walihakikishiwa kuwa majina yao yatahifadhiwa na kutakuwa na usiri mkubwa kwa yale watakayosema. Watoto na vijana hao walijulishwa kwa ufupi maudhui ya utafiti na wakapewa fursa kuwa iwapo wanapenda wanaweza kuamua kutoshiriki katika utafiti. Usalama wa watafiti ulizingatiwa wakati wa kutafiti.

**Maisha kabla ya kuja mitaani: Familia na Nyumbani**

## Turusifu

Turusifu aliishi na wazazi wake wote wawili hadi walipotengana na alibaki akiishi nyumbani na mama yake. Siku moja, wakati huo akiwa na umri wa miaka tisa, Turusifu alikuwa akiwasha jiko la mafuta ya taa na mapazia yalishika moto. Mama yake alimpiga sana na kumfukuza nyumbani akimwambia aende kuishi na baba yake. Kwa kuwa hakujua baba yake anaishi wapi, Turusifu alikwenda kuishi mitaani kwenye mji wake, akikaa na kundi la watoto waliokuwa wanalala katika kibanda cha kuonyeshea mikanda ya video.

Mama yake Turusifu aliumwa na akaondoka kwenda katika mji mkubwa zaidi. Turusifu alirejea kwenda kuishi na mama yake na kumtunza hadi kifo chake. Baada ya mama yake kufariki, Turusifu alihudumiwa na baadhi ya kinamama katika eneo walilokuwa wanaishi hadi alipokutana na mjomba wake ambaye alimchukua akaishi na shangazi yake upande wa mama na bibi katika mji mwingine. Baadaye Turusifu alipelekwa na bibi yake kwa babu mzaa baba yake kijijini ili aweze kwenda shule. Hata hivyo, baada ya bibi yake kuondoka, Turusifu alipigwa na babu yake bila huruma na akamkata kwa visu. Alilazimishwa kufanya kazi ya mchungaji wa mbuzi badala ya kuhudhuria shule. Turusifu aliona kuwa hawezi kuvumilia vitendo vya kikatili alivyofanyiwa akaenda kutoa taarifa polisi kuwa yeye ni yatima na kwamba alikuwa na bibi yake katika mji mwingine. Polisi walimpakia Turusifu katika basi linaloelekea katika mji anaoishi bibi yake. Alipofika kule, bibi yake alimwambia arudi kwa babu yake na akampa nauli ya kurudi lakini Turusifu aliendа kwenye mji alikokuwa akiishi kabla ya kuchukuliwa na bibi yake. Alimtafuta na, akampata mjomba wake, ambaye alikuwa mlevi wa kupindukia na hakuweza kumtafutia Turusifu mahali popote pa kuishi. Kwa hiyo Turusifu, akiwa na umri wa miaka kumi, alikuja mitaani ambako ameshaishi kwa miaka saba sasa.

- Watoto walioshiriki katika utafiti huu walitoka katika familia zenye misingi au mifumo mbalimbali ikiwemo familia za mzazi mmoja mmoja na familia zilizokutanishwa tena pamoja. Masuala yatokanayo na misingi au mifumo tofauti tofauti ya kifamilia yanaweza moja kwa moja au kwa namna fulani kusababisha mtoto kuishi peke yake mitaani.

*"Nilifikiri ilikuwa bora zaidi kutengana nao na kuishi peke yangu kuliko kuishi na mzazi mmoja… kwa hiyo nilitengana nao na kuja kuishi mjini na kujaribu kujitafutia riziki na kujilea mwenyewe."*

- Baadhi ya watoto hawakuwajua mama zao kwa kuwa mama hao waliondoka, au walifukuzwa nyumbani. Kina mama walikutwa na matatizo mbalimbali ambayo yalifahamika kwa watoto wao. Katika baadhi ya matukio, wakati huo huo wakiishi mitaani, baadhi ya watoto waliwasaidia mama zao kifedha.

*"Baba yangu alikuwa na mama mwingine, mama mkubwa, ndiyo maana mama yangu aliamua kuondoka nyumbani kwa hiyo tuliachwa kuishi na mama mkubwa. Mama aliondoka na hakurudi tena."*

- Watoto wengi hawakuwajua baba zao. Baadhi ya kina baba walitelekeza familia zao, hivyo kusababisha umaskini katika familia na mazingira magumu kihisia.

*"Maisha nyumbani yalikuwa mazuri lakini baba na mama waligombana. Baba aliondoka… jambo lililofanya maisha kuwa magumu: baba ambaye ndiye mtafutaji wa chakula hakuonekana tena."*

- Masuala na matatizo yanayohusiana na wazazi wa kambo mara kwa mara yana mchango mkubwa kwenye tatizo la watoto kuishi wenyewe mitaani. Wakati ambapo watoto wachache walielezea kuwa na mahusiano mazuri sana na mama zao wa kambo, wengi walielezea kuwa na mahusiano magumu na kutendewa kikatili na wazazi wao wa kambo.

*"Mama alianza kunitendea mambo ya kikatili: alininyima chakula; niliamua kuondoka"*

- Kufuatia kifo cha mzazi, mara nyingi watoto walikuwa tegemezi kwa kaka au dada zao wakubwa. Mara kadhaa walitengana na kaka au dada zao kufuatia kifo cha mzazi au wakati wazazi au wazazi wa kambo wanapotengana. Baadhi ya watoto na vijana walitamani kuwaona kaka na dada zao tena na wengine walirudi nyumbani kutoka mitaani ili kuwatembelea. Kwa kaka au dada zao kuoa/kuolewa iliweza kuleta mabadiliko ya mazingira ya watoto.

*"Sijisikii vizuri (kuishi mitaani) kwa sababu … nakosa kuwa na dada na kaka zangu."*

- Watoto wengi walilelewa na babu na bibi zao, mara nyingi na bibi (nyanya). Baadhi ya watoto waliona kuwa jambo hili ni zuri, lakini kwa wengine hili lilikuwa ni tatizo. Baadhi ya ndugu wengine katika familia pia waliwalea watoto. Hali kadhalika, baadhi ya watoto walikuwa na maoni mazuri juu ya uzoefu wao wa kulelewa na ndugu wa ukoo na wengine walielezea matatizo.

- Matumizi yasiyofaa ya vileo (ulevi) miongoni mwa wazazi na walezi, ukatili majumbani na matatizo ya akili yalikuwa na athari mbaya kwa watoto na mara nyingi yalichangia watoto kutorokea mitaani.

*"Nilikuwa mjini na nikasikia kuwa mama yangu amelazwa hospitali. Nilipokwenda kumwona, nilikuta amekatwa kwa panga… Baba (wa kambo) alimkata mama kwa panga."*

- Mara kwa mara watoto wengi walinyanyaswa na kutendewa ukatili na wazazi na walezi wao. Unyanyasaji (ukatili) wa kimwili uliofanywa kwao ulikuwa ni pamoja na kuchapwa kwa kutumia fimbo, waya au kukatwa na kisu. Unyanyasaji wa kimwili uliofanywa majumbani na mashuleni mara nyingi ulisababisha watoto kutoroka. Watoto wengi wamejisikia kutojaliwa, kukataliwa na kuachwa peke yao kiasi kwamba haikuwa rahisi tena kwao kubaki majumbani. Kunyimwa chakula au haki ya kwenda shule mara nyingi kuliwafanya watoto watoroke nyumbani.

*"Baba yangu alinifungia ndani, akanifunga kwa kamba: hapo ndipo alipoweza kunipiga. … Alinifunga mikono na miguu kwa kamba."*

*"Usiku mmoja alinifungia nje na siku iliyofuata nilikwenda mitaani. Niliporudi (nyumbani) jioni ile, nilipiga magoti kuomba msamaha lakini wakati nimepiga magoti (bibi) alikuja nyuma yangu na kunipiga kwa kutumia waya. Alinipiga sana kiasi kwamba sitasahau."*

- Baadhi ya watoto walifanya kazi kama walezi kwa kuwatunza wadogo zao au wazazi wao wanaoumwa. Mara nyingine mtoto au kijana aliondoka mitaani kwenda kumtunza mzazi wake mgonjwa, na alirudi mitaani baada ya mzazi kufariki.

- Watoto wengi ni yatima jambo linalowafanya wawe katika hatari kubwa zaidi. Baadhi ya watoto yatima waliwekwa katika uangalizi wa jamaa zao ambao hawakuwalea vema.

- Umaskini katika familia una mchango mkubwa katika kusababisha watoto kuishi peke yao mitaani kwa kuwa umaskini huzuia kupatikana kwa mazingira bora ya malezi, wazazi na walezi hushindwa kuwapatia watoto wao mahitaji muhimu na husababisha msuguano katika mahusiano ya kifamilia. Baadhi ya watoto walitoroka nyumbani ili kujikimu na wakatafuta ajira mijini lakini wakajikuta wakiendelea kusumbuliwa na umasikini katika maisha ya mitaani.

*"Mama yangu ameshafariki na sijawahi kumwona baba yangu. …Nilikuwa naishi na shangazi yangu ambaye hakuweza kunitimizia mahitaji yangu na ya watoto wake wote kwa hiyo nililazimika kuondoka."*

- Wakati wakiishi majumbani baadhi ya watoto walipata misaada kutoka kwa wanajamii kama vile chakula, misaada ya kuwawezesha kuendelea na masomo na pia kuwalinda wasipigwe na wengine.

- Baadhi ya watoto bado wana mawasiliano na familia zao wakati wakiishi peke yao mitaani, baadhi yao wakijisikia wana wajibu mkubwa kwa wanafamilia na kila inapowezekana huwapa misaada ya kifedha. Watoto na vijana wachache wamekuwa wakipata misaada kadhaa kutoka kwa wazazi na walezi wao lakini, mara nyingi, wazazi au walezi hao hawakuulizia kuhusu maisha ya watoto wao au hawakuhoji kuwa wanaishije.

*"(Mama) alikuwa ananitafuta. Aliwapatia fedha baadhi ya watu na kuwataka wanikamate na kunipeleleka nyumbani pale watakaponiona. … Mama yangu aliponiona alizimia kwa furaha … na akaniambia nisikimbie tena ila niwe naenda kumwona na kuondoka ."*

*"Mama alikuwa akinitafuta lakini kila mara tulipishana mpaka tulipopotezana"*

- Watoto na vijana walioshiriki katika utafiti waliulizwa mawazo na mapendekezo yao juu ya nini kinaweza kufanywa ili kuboresha maisha ya watoto wa mitaani, hasa kuhusu mambo ya familia na nyumbani. Maoni ya watoto na vijana hao yalilenga katika: kutambua sababu mbalimbali zinazofanya watoto na vijana waishi maisha ya upweke mitaani; nafasi na wajibu wa serikali kuhakikisha kuwa watoto wanadumu kuishi nyumbani; kutoa misaada kwa wazazi ili kukidhi mahitaji yao; ulazima wa wazazi na watoto kuheshimiana na kutendeana vema; na kuwarejesha watoto nyumbani kwa wazazi lakini kuhakikisha kuwa wazazi na watoto wanasaidiwa ili kwamba mtoto abaki nyumbani.

*"Wewe zungumza nao tu kwa kuwa kila mmoja ana tatizo lake. Kila mmoja aliondoka nyumbani kwa sababu ya tatizo tofauti."*

*"Lazima serikali iwe na mipango ya kuwasaidia watoto na vijana kabla hawajafika mitaani."*

*"Ninapenda kusema, wazazi watunze watoto kama kitu chenye manufaa; wasiwatendee kama vile maisha yao ya baadaye ni uchafu. Mtoto ni mtoto. …Ukimtupa mtoto, atajisikiaje? Na wewe, ulimleta mtoto duniani na sasa ni haki na wajibu wako umtunze vizuri … kwa sababu dunia yetu itajengwa na vizazi vyetu vijavyo. "*

*"Lazima muwarudishe watoto nyumbani kwenye familia zao, mzungumze na familia ili wawalee watoto wao na kuishi nao kwa amani; (familia) wasiwanyanyase (watoto) ila wawapende. …Kama mkizungumza na familia, waambie wafikirie mahitaji ya mtoto … ni vema muendelee kuwatembelea mara kwa mara, labda mara mbili au tatu kwa mwezi au kila mwezi ili kuona mtoto anaendeleaje. Mtajenga mahusiano mazuri na wazazi na kufahamu wanaendeleaje. Labda iwapo hali ya maisha nyumbani yamebadilika kidogo, hii itaweza kumfanya mtoto ajisikie vizuri na kutamani kukaa nyumbani."*

**Uzoefu wa kuishi pekee mitaani**

## Turusifu

Turusifu alipokuwa na miaka kumi, wavulana wawili wakubwa walimlawiti alipokuwa anajaribu kulala. Baada ya kulawitiwa, Turusifu alijisikia vibaya sana, akatafuta mtaro ambako alilala kwa siku mbili, akitoka tu kidogo kwenda kutafuta kitu cha kula pale njaa ilipomlazimisha kufanya hivyo. Turusifu anajielezea kama aliyepoteza matumaini yote katika hali yake hii ya maisha.

Muda mfupi baadaye, mtu mmoja mkarimu alimpa Turusifu kiasi kidogo cha hela. Wale vijana waliomlawiti Turusifu waliona kwamba amepewa hela na wakamfuata mtoni ambako, baada ya kununua sabuni, alikuwa akifua nguo zake. Wale vijana wawili walimlawiti tena Turusifu na wakamwibia nguo zake, wakimwacha na nguo za ndani tu. Akiwa amevalia hivi, Turusifu alikwenda kwenye shimo la takataka akajipatia suruali na shati bovubovu. Wale vijana wawili walirudi tena na kujaribu kumlazimisha Turusifu akubali kufanya kile walichomtaka kumfanyia:

*"Wale vijana walirudi tena na kujaribu kunilazimisha niiname ili wanilawiti. Nilikataa; nilipambana nao. Walichukua kisu na kuanza kunichoma nacho magotini."*

Kufuatia majeraha haya, Turusifu alikaa hospitalini kwa muda na aliruhusiwa pale alipoweza kutembea na akarudi mitaani.

Turusifu alianza kukumbia alipowaona wale vijana wawili ili kuepuka kuwa na ugomvi nao lakini walipojaribu kumshambulia, alijibu mapigo kwa ukali ili kujilinda. Mbinu yao ya kawaida ilikuwa kwamba mmoja wao anamshikilia chini Turusifu wakati mwingine anampiga kichwani kwa jiwe apoteze fahamu ili waweze kumlawiti.

*"Kwa kawaida wanakuja wawili, mmoja wao ananipiga kwa jiwe, naanza kutokwa na damu na kupoteza fahamu; ndipo wanaponilawiti."*

Wavulana hao wawili waliomlawiti Turusifu bado wapo mitaani na wameshawalawiti wavulana wengine ambao Turusifu anawafahamu.

Turusifu anaye dada mdogo ambaye aliishi na mjomba wake upande wa mama. Siku moja baba yake Turusifu, ambaye alikuja kwenye mji ambao mwanae anaishi mitaani, alimwendea Turusifu na kumtaka aende akamchukue dada yake ambaye alikuwa na umri wa miaka 13. Turusifu alimweleza baba yake kuwa hana nauli ya kwenda kumfuata dada yake. Baba yake alimwambia kwamba inabidi aombe ombe mitaani hadi apate hela ya kutosha nauli ya kwenda kumchukua dada yake na kurudi naye. Turusifu alianza kuwaza jinsi ya kupata hizo fedha:

*"Nilikutana na rafiki yangu ambaye alikuwa na tabia ya kuiba vioo vya pembeni kutoka kwenye magari. Siku hiyo alinishawishi niende kuiba. Nilimwambia 'Siwezi; sijui jinsi ya kuiba'. Aliniambia atanifundisha. Kwa kuwa nilikuwa na tatizo (kutafuta fedha ili kwenda kumchukua dada yangu), nilikubali. … Nilishawishiwa kujiunga na ile biashara kwa kuona jinsi rafiki yangu alivyojipatia hela upesi na, kwa kuwa nilikuwa na tatizo, nilifanikiwa kuiba vioo vya pembeni vitatu. Kisha niliondoka kwenda kumtafuta dada yangu."*

Turusifu alimdanganya dada yake, akimwambia kuwa baba yao sasa ana nafasi na uwezo mzuri na anaweza kumtunza. Kwa kuwa maisha yake yalikuwa magumu kutokana na kutendewa vibaya na kupewa kazi nyingi, dada yake alifurahia kuondoka. Turusifu alimpeleka dada yake pale alipokuwa akiishi baba yao na yeye aliambiwa na baba yake arudi mitaani. Turusifu alipata kazi ya kuhudumia bustani na alifurahia kujishughulisha, akiiona hii kama njia ya kumaliza matatizo yake. Siku moja alijisikia tu kwamba kuna kitu ambacho hakiko sawa na aliamua kutofanya kazi ila akamtembelee baba yake. Alipofika, Turusifu aliambiwa kuwa dada yake yupo kwa mjumbe wa nyumba kumi (balozi), na kwamba baba yake amepelekwa kituo cha polisi baada ya kumbaka dada yake Turusifu. Ili kupata ushahidi, dada yake Turusifu alipelekwa hospitali ili vipimo vichukuliwe.

Baada ya baba kumbaka dada yake, Turusifu aliendelea tena kuiba vioo vya pembeni vya magari ili aweze kupata hela za kumlipia dada yake apate matibabu. Baadaye, Turusifu alitambua kwamba kuiba *ni vibaya na ni hatari:*

*"Kwa hiyo nilikaa mitaani na kutambua kuwa iwapo nitaendelea kuiba vioo vya magari, ni vibaya na naweza kuishia kuuwawa. Niliamua kujishughulisha na biashara ndogondogo na kidogo ninachopata naridhika nacho, kwa mfano sasa nauza mifuko ya plastiki na natafuta vyuma chakavu ambavyo nauza."*

Vipimo vya hospitali vilithibitisha kuwa dada yake Turusifu alibakwa, kwa hiyo Turusifu na dada yake walikwenda polisi. Turusifu na dada yake waliambiwa warudi siku iliyofuata ili baba yao apelekwe mahakamani. Kama walivyoombwa, Turusifu na dada yake walienda kumwona mjumbe wa nyumba kumi ili awasaide zaidi. Walifanya hivyo, na baadhi ya wazee walikuja kuwaona na kuwashawishi wasiendelee kusisitiza baba yao afunguliwe mashtaka. Waliwaelezea jinsi ambavyo baba yao hatakubaliwa kupewa dhamana, kwamba atapelekwa kifungoni; kitu ambacho kinamaanisha wataachwa wenyewe bila baba kwa sababu anaweza kufia gerezani na watawajibika kumzika. Turusifu na dada yake walikataa kuridhia matakwa ya wale wazee lakini baada ya kumtembelea baba yao na kumkuta amekonda sana walifikiri anaweza kufa na wakaamua kumsamehe. Turusifu alitambua kuwa si yeye wala dada yake ambaye angeweza kukaa na baba yao na wakamtafuta mfanyakazi mwenye huruma kutoka katika kituo kile alichoishi ili amsaidie kutafuta mahali ambapo dada yake atakaa. Huyu mfanyakazi alikubali kwamba dada yake anaweza kukaa naye. Hapa ndipo dada yake anaishi hadi sasa na anahudhuria shule wakati Turusifu bado anaishi mitaani. Turusifu alielezea jinsi kitendo cha dada yake kubakwa na vitendo vya kulawitiwa alivyofanyiwa yeye mwenyewe vinavyomtia hasira na kumkosesha amani. Mara nyingine Turusifu anajisikia mnyonge sana na analia.

- Uzoefu wa kufika mitaani ulitofautiana sana kati ya mtoto na mtoto. Baadhi ya watoto walikaribishwa na watoto wenzao na vijana na wakapewa ushauri jinsi ya kukabiliana na maisha wakati wengine walikumbana na vitendo vya fujo na ukatili.

*"Ilikuwa vizuri. Nilikaribishwa vizuri … na marafiki zangu (ambao tulifahamiana mitaani). Tulikutana hapa na tukaanza kutembea pamoja."*

*"Nilichukuliwa (na polisi) na kupigwa. Niliambiwa nisirudi tena mitaani."*

- Baadhi ya watoto na vijana waliona tofauti ndogo kati ya kuishi peke yao mitaani na kuishi nyumbani.

*"Kwangu ni sawa tu : hapa (kuishi mitaani), nyumbani."*

- Uamuzi wa nani wa kuishi naye ni mkakati muhimu wa kumudu kuishi. Vijana wengi na watoto waliunda vikundi kuimarisha usalama na ulinzi wao, kuweka utambulisho na kujihakikishia uwezo wa kuichumi, lakini wengine walipendelea kuishi peke yao.

*"Nilipendelea tu kuishi peke yangu. ...Nilijiepusha kukaa na marafiki nisije kuishia kuchukuliwa na polisi."*

- Kuwa mjanja na mtukutu, mdanganyifu na kuweza kupigana ni tabia zinazowasaidia vema watoto na vijana wanapoishi peke yao mitaani.

*"Kuwa na uzoefu mzuri wa kupigana; hiyo ni muhimu kwa maisha ya mitaani."*

- Wengi wanafanya kazi ambazo haziwahakikishii kupata kipato chochote kama vile kubeba mizigo na vifaa vingine au kukusanya na kuuza vyuma chakavu, kuni, mkaa na chupa. Baadhi ya vijana na watoto waliweza kujipatia kiasi kidogo cha pesa mara kwa mara kwa kufanya kazi zenye uhakika zaidi.

> *"Nakwenda, natafuta gunia na kuchukua kuni… Naenda kuziuza; nikishaziuza, nakwenda kuhifadhi hiyo hela mahali halafu naunganisha na nyingine nanunua nguo na pipi … halafu nauza."*

- Wizi ni mkakati au mbinu ya hatari kutumia ili kuishi na inaweza kuwa na madhara makubwa sana kwa mtoto au kijana akikamatwa au kutuhumiwa kuiba. Watoto na vijana pia huibiana. Wengine hawaibi ila kuna kila sababu ya kuamini kuwa wataanza kuiba iwapo wataendelea kuishi mitaani.

> *"Inabidi uibe kwa sababu huwezi kuwa na uhakika utapata chochote (hela) lini."*

- Kuombaomba ni mbinu iliyozoeleka ya kuishi mitaani kwa watoto ambao mara nyingine huitumia kama ndiyo njia pekee ya kujipatia fedha na chakula. Kuombaomba pia huweza kutumiwa na vijana na watoto wakubwa wakati mbinu nyingine za kujipatia fedha zinaposhindwa. Wale ambao wanategemea tu mbinu ya kuombaomba wanaweza kuishi kwa kipindi fulani bila kitu chochote cha kula.

> *"Mara nyingine ninaposikia njaa, naenda kuomba kwa mtu."*

- Watoto na vijana mara nyingine hutafutana na ingawa bila mafanikio, huwashawishi watoto wenye umri mdogo kurudi nyumbani.

> *"Huwa tunawaambia waende nyumbani; tunawalazimisha waondoke mitaani warudi nyumbani.*
>
> *…Hao wakubwa mara kwa mara hutulazimisha turudi nyumbani. …Wale wazuri (miongoni mwa vijana wakubwa) ndio hutushawishi turudi nyumbani."*

- Watoto wengi na vijana wanatumia vitu vya kulewesha, hasa gundi, kama mbinu ya kuwawezesha kuishi peke yao mitaani na kuwapunguzia ugumu wa maisha wanayoishi huko. Mara nyingi watoto na vijana wanashawishiwa na wenzao kuanza kujaribu madawa au ulevi mwingine ambao wanatumia. Baadhi ya watoto, baada ya kutambua madhara ya kutumia gundi, wameacha kutumia ingawa baadhi yao wanatamani, wameshindwa kuacha. Imeonekana kama vile kutumia gundi ni kitu kisichoweza kuepukika, hasa iwapo mtoto au kijana anakaa mitaani kwa kipindi kirefu.

> *"(Unapotumia gundi) husikii njaa."*

- Kuamini kilichopangwa kitatokea ni jambo la kawaida na imani ya kijana au mtoto inaweza kuwa muhimu kumwezesha kuishi mitaani na kudumisha mtazamo mzuri kuwahusu wao wenyewe au mazingira wanayoishi. Masuala ya uchawi na ushirikina yanatumika pia kuelezea sababu ya kwa nini wanajikuta wanaishi peke yao mitaani.

- Watoto na vijana walielezea kupokea misaada kutoka kwa watu wengine katika jamii. Misaada mingine hutolewa tu kwa ahadi au kujifanya kuwa watoaji watatoa ingawa hawafanyi hivyo. Baadhi walielezea kupata misaada kutoka kwa Wazungu8 lakini hili huweza kuwasababishia usumbufu watoto au vijana wenyewe au watu wanaotaka kufanya kazi na watoto au vijana.

> *"Tulishangazwa sana baadaye kuona jinsi alivyotutelekeza. … Nilijisikia vibaya sana."*

- Ukatili na ugomvi daima upo mitaani na watoto na vijana wanaweza kwa wakati mmoja au mwingine kuwa wahanga au waendelezaji wa ukatili na ugomvi huo. Watoto na vijana wanaweza kufanyiwa ukatili au ugomvi na wenzao wanaoishi nao mitaani; vijana wakubwa wa kiume mara nyingi ndio waendelezaji wa ugomvi na vitendo vya ukatili kwa watoto wadogo. Vitendo vya kikatili pia vilielezwa kufanywa na polisi, maafisa wengine na walinzi.

> *"Kulikuwa na kijana mmoja ambaye wakati fulani aliniambia ataniua siku moja iwapo atanikuta nimelala: alikuwa ananilazimisha nimpatie hela niliyopata."*
>
> *"Watu wa manispaa na polisi wanatupiga usiku."*
>
> *"Tunawaogopa sana polisi."*

- Watoto wengi wa kiume walielezea kulawitiwa kwa nguvu na watoto wa kike walikumbana na kubakwa au jaribio la kudhalilishwa kingono,. Mara nyingi kuna tofauti ndogo sana kati ya ngono ya kuridhia na kubakwa kati ya wanaume. Kudhalilishwa kingono mara nyingi kulisababisha mtu kujisikia kuvunjiwa sana heshima na kuumiza hisia. Baadhi ya vijana wakubwa walijaribu kuwapatia ulinzi watoto wadogo ili wasidhalilishwe kingono. Kulikuwa na hali ya kuzoea vitendo vya udhalilishaji wa kingono. Kutekeleza uhalifu kwa kubaka kunaweza kuonekana kama namna ya kuonyesha nguvu na hasira. Mwenendo wa tabia za kingono na udhalilishaji wa kingono kunaongeza wasiwasi kuhusu maambukizi ya VVU / UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa, afya ya akili, maendeleo ya kijinsia na mahusiano ya kimapenzi..

> *"Wale wakubwa wanakuja kwenye eneo letu na kufanya ngono na watu, hasa watoto wadogo."*
>
> *"Ukilala maeneo ya wazi nje, unaweza kukamatwa na baadhi ya walinzi wenye tabia mbaya …. Mlinzi anaweza kukulawiti wakati umelala."*

- Watoto wengi na vijana wanakabiliwa na matatizo ya kiafya yanayotokana na majeraha, magonjwa na kupigwa. Matatizo mengine ya kiafya pia yanatokana na lishe duni na mazingira mabaya ya kuishi. Matatizo ya afya ya akili pia yalionekana.

> *"Unachambua katika shimo la takataka kutafuta kitu cha kula … na kusumbuliwa na matatizo makubwa ya tumbo kama maumivu ya tumbo, kuharisha na mara nyingine unaweza kulala chini ukihangaika kwa maumivu."*

- Maisha ya watoto na vijana yanaweza kuchukua uelekeo tofauti tofauti wakati wakiishi mitaani. Baadhi ya watoto na vijana wanaonekana kumudu kuishi vizuri zaidi kuliko wengine; baadhi ya watoto na vijana wanaonekana kujenga uvumilivu zaidi na kumudu zaidi kuishi maisha ya mitaani kadiri muda unavyoendelea na wakati huo wengine wakiendelea kukumbana na vurugu na unyanyasaji. Kwa baadhi, hakuna badiliko katika maisha yao ya mitaani katika kipindi cha miaka mingi. Baadhi ya vijana wakubwa hawalali tena mitaani ila maisha yao bado yana uhusiano na mitaani. Baadhi ya watoto na vijana walikuwa na malengo/matamanio ya kimaisha ambayo ni tofauti sana na mazingira wanayoishi kwa sasa.

*“Labda nitakuwa kama Barack Obama na kuwa Rais.”*

- Mapendekezo kutoka kwa watoto na vijana yalilenga kwenye: kuamsha uelewa juu ya huduma za msaada kwa watoto wanaoishi wenyewe mitaani; kuwapatia misaada ili kukidhi mahitaji yao; misaada hiyo itolewe na watu mbalimbali kwa kusaidiana na serikali; kutoa mafunzo na fursa za ajira; kuwa na upendo kwa watoto na vijana; kuhakikisha kuwa vituo vya malezi vina uwezo wa kuwahudumia watoto na vijana wanaotunzwa humo; kutoa misaada mahsusi kwa wasichana; kutambua kuwa ni vigumu au haiwezekani kuwahudumia watoto na vijana wote waishio mitaani; na kuwaelimisha watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani ili waishi kwa kupendana badala ya kupigana.

*“Mimi nafikiri tu kwamba hawa watoto (wanaoishi mitaani) wangepelekwa kwenye vituo vya kulelea yatima na itangazwe kwenye runinga (TV) au kwenye redio ili kwamba hao wasiofahamu wajue nyumba za watoto yatima zilipo.”*

*“Ningependa kuiomba (serikali) itujengee mahali salama tunapoweza kuishi.”*

*“Wapelekwe shule ili maisha yao ya baadae yawe mazuri.”*

*“Napenda kuwaelimisha hao wanaopigana ili kwamba kama tunaendelea kukaa (kuishi mitaani), tuweze kuishi kwa amani, kuishi kwa upendo.”*

**Uzoefu wa Watoto na Vijana kuhusu Mashirika yanayowahudumia**

## Turusifu

Baada ya kuishi mitaani kwa miaka miwili hivi bila kupata msaada wowote ili aweze kuondoka katika maisha ya mitaani, Turusifu aliamua kwenda katika kituo cha watoto wanaoishi mitaani. Wakati anaishi kituoni, Turusifu alijikuta katika matatizo na kijana mmoja mkubwa ambaye alikuwa akiishi pale pia:

*“Mmoja wao kwa kweli alipenda sana kunionea. Kila mara tulipopewa kazi za kufanya, alinisukumia kila kitu nifanye mimi: kudeki na kuosha vyombo. Nilijisikia kama vile natumikishwa.”*

Pale kituoni watoto walipewa mafunzo ya kujilinda na kujitetea kwa njia ya kupigana. Turusifu hakuyapenda mafunzo haya ya kujilinda na kujitetea kwa sababu mara nyingi mwalimu alikuwa akiwaumiza watoto:

*“Sikuridhika na hili kwa sababu mwalimu alikuwa na kawaida ya kumpiga kofi mtu yeyote ambaye anakosea kufanya kama alivyofundisha. Siku moja nilipatwa na maumivu makali sana ya kichwa, alinipiga sana. Nilikasirika sana na niliondoka kurudi mitaani.”*

Turusifu hajatafuta tena kuishi kituoni tangu aliporudi mitaani lakini anapenda kupewa msaada wa mafunzo ili apate ujuzi, apate kazi, aondoke mitaani baada ya kujipatia kipato na aweze kujitafutia mahitaji yake.

- Katika maeneo yote manne ambapo utafiti ulifanyika kulikuwa na msaada maalumu kwa watoto na vijana wanaoishi mitaani. Hata hivyo, aina ya misaada iliyotolewa ilitofautiana kila mahali.

- Watoto na vijana hawakuweza kupata misaada kwa sababu hawakuwa na habari juu ya kuwepo kwa misaada hiyo katika eneo wanaloishi; misaada iliyotolewa haikulingana na mahitaji yao; hawakufurahia jinsi misaada hiyo ilivyotolewa; au hawakupewa kabisa misaada hiyo.

*“Sijaona msaada wowote.”*

*“Sijui inakopatikana. … Ningelijua ningekwenda.”*

*“X (jina la shirika)? Hawajafanya chochote kwa ajili yangu”*

- Wakati huduma za malazi ziliposimamishwa, watoto na vijana walilazimika kurudi mitaani.

- Baadhi ya watoto na vijana hawakuweza kupatiwa huduma baada ya kuonyesha tabia zisizokubalika.

- Baadhi ya mashirika au vituo vina uhaba wa rasilimali za kutosha kukidhi mahitaji ya watoto na vijana wanaowahudumia.

- Gharama za shule kwa baadhi ya watoto na vijana wanaokwenda shule ni kubwa na hii huweza kusababisha misuguano na ugomvi kati ya watoto na wazazi au walezi wao.

*“Baba alikataa kunilipia hela ya mitihani. …alikataa … na akaniambia ‘Nitakupiga!’ Kwa hiyo, siku ya mitihani, nilibaki nje (ya shule) pamoja na watoto wengine ambao nao hawakuweza kulipia.”*

- Baadhi ya watoto na vijana hawajawahi kabisa kwenda shule lakini wengi wameshaenda shule kwa kipindi kifupi.

- Elimu inathaminiwa sana na watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani.

*“Kupata elimu ndicho kitu kitakachonisaidia.”*

*“Ninapenda kwenda shule.”*

*“Maisha hayatakuwa mazuri nisipopata elimu.”*

- Ukosefu wa huduma za bure za afya unaweza kuwanyima baadhi ya watoto na vijana fursa ya kupata matibabu wanapokuwa wagonjwa au wamepata majeraha. Kupewa rufani kutoka katika mashirika ya misaada yanayowahudumia watoto na vijana wa mitaani kunaweza kuwasaidia kupatiwa huduma za kiafya, ingawa ubora wa huduma zinazotolewa mara nyingi umeelezwa kuwa wa hali ya chini.

*“Pale hospitalini, hawakunitibu vizuri sana. Waliniosha tu kidonda na kuniwekea bendeji. … Walitaka nilipe pesa na mimi sikuwa na pesa.”*

- Baadhi ya watoto na vijana hukamatwa na kufungwa katika mahabusu ya polisi au katika vituo vya magereza. Mara nyingi watoto na vijana huchanganywa na watu wazima. Ukatili na unyanyasaji kingono vimeripotiwa kufanyika katika nyumba hizi za mahabusu.

*“Nilifungwa pamoja na watu wazima.”*

*“Kulikuwa na kupigwa sana pale (mahabusu ya watoto). Nilitoroka.”*

- Pamoja na kwamba baadhi ya sifa nzuri zilitolewa kuhusu kuishi katika vituo, watoto wengi na vijana hawakupendelea maisha ya kwenye kituo kwa sababu hawakuweza kufikia matarajio au mahitaji yao; walilazimishwa kufanya kazi ngumu; walijisikia kunyanyaswa na wafanyakazi na kufanyiwa vitendo vya kikatili na watoto au vijana wenzao; au walikuwa na fikra kuwa baadhi ya wafanyakazi walikuwa wakitumia vibaya rasilimali za kituo. Watoto na vijana pia walielezea jinsi walivyopatiwa elimu katika kituo, elimu ambayo ni ya kiwango cha chini sana ukilinganisha na uwezo wao.

*"Nilitoroka katika kituo kile kwa sababu hapakuwa na chakula cha kutosha pale."*

*"Kitu kimoja kilichonifanya nisikae pale (kituoni) ni kwamba tulikuwa tunaamka asubuhi mapema na kulima shamba wakati shule zimefungwa. Tulikuwa tunalima kweli kweli na ulikuwa unaweza kupigwa kama ukibaki nyuma ya wenzako wakati wa kulima."*

*"Sisi pale (kituoni) tulikuwa tunajifunza. Tulikuwa tunaandika vizuri, tunafanya vizuri na kuongoza darasani lakini ilikuwa kama darasa la chekechea."*

- Kwa hakika baadhi ya watoto na vijana wanapata ugumu sana kuishi vituoni wakibanwa na sheria na mipaka hasa baada ya kuwa waliwahi kuishi mitaani wakiwa na uhuru wa kiasi fulani.

- Mara nyingi watoto na vijana hawakufurahia huduma walizopata kutoka kwa mashirika ya misaada ikiwa na nia ya kukidhi haja zao kwa kuwa hawakuweza kujionea wenyewe na kuhakikishiwa kuwa mashirika hayo yalikuwa yakitimiza ahadi zao na kwamba mabadiliko ya kudumu ya maisha yao yangepatikana kutokana na mipango ya misaada inayotolewa kwao.

*"Nilipofuatilia, niliambiwa kuwa hawa watu hawapo tena hapa mjini; wamehama na kwamba ningeweza kuwapata karibu na barabara hii lakini sikuwaona. Ilibidi niishie tu hapo hapo. … Sina hamu tena."*

- Mapendekezo ya watoto na vijana yalilenga kuhakikisha kuwa watoto na vijana waishio mitaani wanapata elimu na kwamba wafanyakazi katika vituo vya misaada hawajihusishi na vitendo vyovyote vya ubadhirifu.

*"Ni muhimu wajenge kituo cha watoto kwa ajili ya malezi ya watoto na pia kuwapatia elimu."*

*"Wasiwaweke watu wabadhirifu katika hizo taasisi."*

### Mahusiano, utambulisho na Ustahimilivu

- Uzoefu wa watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani, kabla na wakati wanapoishi wenyewe mitaani, unaonyesha kuwa kuna madhara makubwa yanayohusiana na kuwa na mahusiano yasiyo salama na yasiyo ya kudumu ambayo yanaweza kumfanya mtoto au kijana kuwa na tabia ya ukatili, kuharibikiwa kisaikolojia na kudhoofisha makuzi yake kwa ujumla na kwa hiyo kuathiri mahusiano yake na watu kwa siku zijazo.

- Umuhimu wa maendeleo ya kujitambua unafahamika. Umri wa kati wa utoto na ujana hasa wakati wa balehe ni wakati wa mabadiliko makubwa ya kimaumbile na kiakili ambayo yanamfanya mtoto kujipa utambulisho wake. Watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani wanalazimika kukumbana na mabadiliko kama vile kujitegemea katika umri mdogo kuliko wengine na mara nyingi hawapati msaada wowote wa kuwaongoza jinsi ya kukabiliana na mabadiliko hayo.

- Maendeleo ya kujitambua kiundani yanaweza kuwa tatizo kutokana na matatizo ya kimahusiano wanayokabiliana nayo watoto na walezi au ndugu zao, hasa kufuatia vifo vya wazazi wao na kukosa ile hali ya kuwa na makao maalumu jambo linalowakabili watoto na vijana wengi wanaoishi peke yao mitaani.

- Kuishia katika mazingira ya mitaani kuna athari katika maendeleo ya kujitambua kwa mtoto au kijana, kama ambavyo pia matendo anayotendewa na wenzake yanavyoweza kumuathiri.

- Watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani mara nyingi huonyesha uvumilivu na uwezo wa hali ya juu wa kukabiliana na matatizo licha ya kutokuwa na vitu vingi vya kuwakinga na kuwasaidia maishani mwao.

### Maoni ya kuhitimisha

Mambo mbalimbali yanaweza kusababisha watoto kujikuta wanaishi peke yao maisha ya mitaani nchini Tanzania na Kenya, ikiwa ni pamoja na umaskini, ugomvi kati ya wazazi au walezi, kifo cha mzazi au mlezi na mambo yanayohusiana na shule, au kukosa fursa ya kwenda shule.

Mitazamo na jinsi watoto wanavyotendewa nchini Tanzania na Kenya vina mchango juu ya jinsi watoto wanavyojikuta wanaishi wenyewe mitaani na jinsi wanavyotendewa pale wanapoishi mitaani. Mchakato wa kufanya kazi za nje/mitaani nchini Tanzania na Kenya na matokeo ya utafiti umeonyesha kuwa watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani wanatazamwa na kutendewa kwa namna mbalimbali na maofisa na wanajamii wengine. Mitazamo hii mara nyingi husababisha watoto na vijana hawa kuonekana kama tatizo la kijamii, jambo linalohalalisha vurugu na udhalilishaji wa kingono dhidi yao, mambo ambayo ni vigumu sana kutendewa watoto na vijana wengine. Baadhi ya vitendo wanavyofanyiwa watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani vinadhalilisha utu wa mwanadamu; hili linaweza kuonekana kwa jinsi ambavyo wanavyotazamwa kama 'tatizo' na katika mashtaka wanayosomewa kama vile ya 'kuchafua', mambo ambayo yanawafanya waonekane zaidi kama vitu na wala si wanadamu.

Lipo hitaji la kuamsha ufahamu ndani ya taasisi zenye jukumu la kuwalinda watoto ili kuwakumbusha wajibu wao chini ya sheria za kitaifa na kimataifa, lakini pia kuwaelimisha juu ya mazingira yanayopelekea watoto na vijana waishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya. Upo pia umuhimu wa

kuamsha ufahamu ndani ya jamii ambapo watoto na vijana hutokea, na jamii ambazo watoto na vijana hawa hujiingiza pale wanapoingia katika maisha ya kuishi mitaani.

Kuhalalisha vitendo vya kikatili dhidi ya watoto na vijana ni sababu ya msingi inayowafanya watoto na vijana kukimbilia mitaani na hata yale wanayokumbana nayo mitaani. Vitendo vya kikatili ambavyo watoto wanaviona au kutendewa majumbani vinaweza kuwasababisha waishi maisha yasiyo salama na kujiunga na vikundi visivyo salama. Watoto wengi pia hutendewa ukatili wawapo mashuleni. Mitaani, maisha yaliyojaa vitendo vya kikatili huendelea. Ukatili wa kingono pia hufanyika pamoja na hofu zinazoandamana na vitendo hivyo ikiwa ni pamoja na madhara ya kiakili na kimwili, na mahusiano ya baadae ya kimapenzi.

Ipo haja ya kuamsha ufahamu na kutambua madhara ya ukatili dhidi ya watoto: hofu na mateso vinavyosababishwa na ukatili, athari zake katika kuunda mahusiano yasiyo salama na yasiyo sahihi ambayo ni chanzo cha matatizo kwa watoto na hali yao ya kulea watoto siku zijazo na pia athari kwa jamii kwa ujumla. Ufahamu huu lazima uanzie ngazi ya kitaifa na kila aina ya ukatili unaoidhinishwa na taifa dhidi ya watoto ikiwa ni pamoja na adhabu ya viboko lazima ikomeshwe.

Baadhi ya watoto na vijana walioshiriki katika utafiti walisema kuwa vitendo vya ukatili wa kingono vilishakuwa sehemu ya kawaida ya maisha yao. Ni muhimu kujitahidi kujenga mazingira ya kuaminiwa na kuhakikisha kuwa watoto na vijana wanajisikia salama ili waweze kukujulisha masuala yao ya kulawitiwa kwa nguvu na hata kuomba msaada. Ni muhimu pia kuamsha ufahamu miongoni mwa watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani ili kuwasaidia kujitunza katika hali ya usalama kadiri wawezavyo na kujiepusha na vitendo vya kudhalilishwa kingono na kujihusisha na ngono zilizo salama.

Watoto na vijana waishio peke yao mitaani wanaonyesha mbinu na mikakati mbalimbali ya jinsi ya kumudu maisha hasa kwa kujitafutia maarifa ya kukabiliana na mazingira ya hatari sana au fujo. Mambo mengine mazuri ni pamoja na jinsi wanavyowatunza wale ambao wanaonewa, kuwazuia baadhi yao wasiwadhuru wengine na pia jinsi wanavyofanya kazi kwa bidii si kwa ajili ya kupata mlo wa siku hiyo tu bali pia wanaweza kuzitunza familia zao nyumbani kwa kuwapatia chakula na fedha.

Elimu ni muhimu sana kwa watoto na vijana. Kuwanyima fursa ya kuhudhuria shule ni miongoni mwa sababu kubwa zinazowafanya watoto na vijana kutoroka nyumbani na kwenda kuishi mitaani. Watoto na vijana wanaoishi mitaani wanatamani sana kupata elimu na wameielezea kuwa ni muhimu katika kumwezesha mtoto au kijana kuondokana na maisha ya kuishi mitaani. Kiu kubwa ya elimu ambayo imeonekana wazi miongoni mwa watoto walioshiriki katika utafiti huu inaweza kutumiwa kama mbinu au nyenzo ya kuwashirikisha watoto na vijana. Hata hivyo, ni muhimu kwa mashirika na taasisi zinazojijihusisha na watoto na vijana hawa kutambua kuwa mtoto au kijana anayepatiwa msaada huo wa kielimu anaweza kuacha kuendelea kujifunza iwapo msaada huo wa kielimu anaopatiwa ni wa kiwango cha chini kuliko anavyotarajia.

Zipo tofauti za kimaisha miongoni mwa watoto na vijana nchini Tanzania na Kenya kabla ya kuja mitaani na wakati wakiishi mitaani, na pia kuna mambo ambayo uzoefu unafanana. Ni muhimu kwa watoa huduma kutilia maanani uzoefu wa watoto na vijana wanaoishi mitaani wenyewe kwa muda mfupi na wale ambao wanaishi mitaani kwa muda mrefu. Wasichana na vijana wadogo wanakabiliwa na athari za kipekee wanapoishi peke yao mitaani, kwenye vituo vya watoto au wakitumika kama wafanyakazi wa nyumbani (hausigeli) au kwenye ajira nyingine ili kuepuka kuishi mitaani. Ni muhimu kwa hiyo kuandaa huduma mbalimbali na mahsusi ili kukidhi mahitaji na ulinzi wa watoto wa kike.

Huduma zinazotolewa kwa sasa zinatoa fursa ya kutatua tatizo hili kwa viwango tofauti katika maeneo tofauti ya miji; rasilimali zaidi zinapaswa kutolewa kwa taasisi na mashirika yanayohudumia watoto wa mitaani ili kuzipa fursa ya kutoa huduma mbalimbali katika miji yote ambapo kuna watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani. Huduma zinazotolewa lazima zilenge kusaidia kutatua matatizo ya msingi ya kimaisha kama vile, mahali pa kuishi, chakula, huduma za kiafya na mavazi, kutoa msaada wa kielimu, mafunzo au uzoefu wa kazi utakaomwezesha mtoto kujitegemea. Ni vema ieleweke kwamba uzoefu na mambo wanayokabiliana nayo watoto na vijana waishio mitaani vinaweza kuwafanya wapungukiwe au wakose imani kwa watu wengine. Wale wanaofanya kazi na vijana waishio peke yao mitaani wana jukumu la kutoa muda na kujenga urafiki na mahusiano kwa njia ya kuwasikiliza watoto na vijana hao ili nao wajenge kuwaamini, ndipo misaada yao itakapopokelewa.

Kazi za kuwahudumia watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani zinaweza kuandamana na hatari fulani fulani. Kutokana na hatari hizo na masuala ya watoto na vijana hao, ni muhimu kwa hiyo kuhakikisha kuwa wale wanaofanya kazi na watoto na vijana hao wanasaidiwa kikamilifu ili kuwahakikishia usalama wao wa kimwili na kiakili.

Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha jinsi majaribio yenye nia njema ya kuwapatia misaada watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya, yasipotimizwa , yanavyoweza kuharibu na kuwavunja moyo watoto na vijana ambao wanakuwa wameamsha matumaini, wakiamini kuwa baada ya muda mfupi wataishi maisha bora na ya tofauti, badala yake wanajikuta wamekumbana na tatizo jingine jipya la kutelekezwa au kutokubalika.

### Hatua muhimu kwa ajili ya Sera, Utekelezaji na Utafiti

- Matokeo ya utafiti huu yanaonyesha kuwa watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya hawapati haki nyingi zinazoelezewa katika sheria na sera za Tanzania na Kenya, ziwe zile za ndani au za kimataifa. Ili kuhakikisha kuwa watoto na vijana wanapatiwa haki zao ni lazima kuhakikisha kuwa hatua zifuatazo zinachukuliwa:

#### Sera na Sheria ya Kimataifa

  - Viashiria maalumu lazima viongezwe katika kupima mafanikio ya Malengo ya Maendeleo ya Milenia ambavyo vinahusiana na watoto na vijana wanaoishi mitaani.
  - Lazima kuwe na vyanzo maalumu vya fedha kwa watoto na vijana walioko mitaani kwa ajili ya msaada wowote wa maendeleo unaowalenga watoto
  - Lazima kuwe na vyanzo maalumu vya fedha kwa mashirika ya maendeleo ya kimataifa yanayotambua hitajiko la utatuzi wa kina kwa watoto walioathiriwa na ukatili.

### Sera za Kitaifa

- Mchakato ulioainishwa katika sheria ya kuandikisha vituo vya watoto uangaliwe upya na tume maalum iteuliwe kufanya ukaguzi na kuhakikisha kuwa sheria zinazingatiwa.
- Kulingana na Azimio la Baraza la Umoja wa Mataifa la Haki za Binadamu juu ya Watoto wa Mitaani 2011, serikali zote mbili zinapaswa kuwa na sera na kuhimiza utekelezaji unaozingatia kuwa 'mbinu za kujikimu kimaisha kwa mfano kuombaomba, kuzurura, kutokuwa na makazi, utoro shuleni, kutoroka nyumbani na matendo mengine, yanashughulikiwa kwa kuzingatia kuwa ni masuala ya ulinzi wa watoto na kuhakikisha kuwa sheria zinazotungwa kushughulikia tabia za namna hiyo haziwi kikwazo katika kutoa msaada unaotakiwa.'
- Sera zote za kitaifa zinazowahusu watoto, kwa mfano zile ambazo zinashughulikia vikwazo katika kufikia elimu kwa wote, yatima na VVU/UKIMWI, lazima ziwe na kipengele mahsusi cha mahitaji maalumu ya watoto na vijana waishio mitaani na kuainisha kwa uwazi jinsi mahitaji yao yatakavyopatikana.

### Kwa namna ya kipekee kwa Tanzania:

- Katika Mpango Kazi kwa ajili ya Watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (National plan of Action for Most Vulnerable Children), Kamati za Kuhudumia Watoto wanaoishi katika Mazingira Hatarishi (MVCCs) nchini Tanzania zinapaswa kupewa jukumu la kuwatambua watoto waliopotea kutoka katika jamii zao na kuyasaidia mashirika ya kijamii (CSOs) na Ustawi wa Jamii katika juhudi zao za kuwarejesha nyumbani. Halikadhalika, katika kuwatambua watoto walio hatarini katika jamii zao ambao wanaweza kupatiwa misaada na huduma zinazotajwa katika Mpango wa Utekelezaji, MVCCs inapaswa kupanua viashiria vinavyotumika kuwatambua watoto walio hatarini ili kuwahusisha watoto wanaoishi katika familia zenye vitendo vya kikatili na familia zisizoweka mkazo wa kutosha katika malezi ya watoto.
- Mpango kazi wa kitaifa wa kupambana na kushughulikia madhara ya ukatili kwa watoto (The National Response to Violence against Children in Tanzania) unapaswa kuhakikisha kwamba mambo waliyokumbana nayo watoto na vijana wanaoishi peke yao mitaani yanapatiwa ufumbuzi na sekta mbalimbali zinachukua hatua za kuzuia na kutatua ili kukidhi mahitaji ya watoto na vijana.
- Mpango Mkakati kwa Watoto waishio Mitaani nchini Tanzania upitiwe mara kwa mara ili kuhakikisha kuwa unalingana na uzoefu na uhalisia wa maisha ya watoto wanaoishi mitaani na kwamba unakidhi mahitaji yao.

### Kwa namna ya kipekee nchini Kenya:

- Watoto na vijana waishio peke yao mitaani wanapaswa kutambuliwa na kuhudumiwa kulingana na Sera ya Taifa kuhusu Watoto Yatima na Watoto walio katika Mazingira Hatarishi.

### Utekelezaji

- Itifaki na miongozo lazima iandaliwe kati ya polisi, ustawi wa jamii/idara za watoto na mashirika ya kijamii, itafiki na miongozo hii ielezee kwa uwazi hatua sahihi zinazopaswa kuchukuliwa kwa watoto na vijana wanaoishi mitaani na jinsi kila idara/taasisi itakavyofanya kazi kwa kushirikiana na nyingine ili kufahamu na kuyatimiza mahitaji ya watoto na vijana hao. Wafanyakazi wanaotoa huduma mitaani ni lazima wawe sehemu muhimu kabisa ya hatua sahihi zinazopaswa kuchukuliwa.
- Utatuzi wa kina kulingana na mazingira ya Kenya na Tanzania ni lazima uandaliwe kwa ajili ya watoto na familia zao, utatutuzi huo utambue athari za ukatili na kupunguza athari za ukosefu wa usalama na mahusiano yasiyo sahihi.
- Majibu ya kiutendaji lazima yaainishwe kukidhi mahitaji ya wazazi na misaada itolewayo kwa wazazi na pia kwa wana familia wengine ili kuwezesha malezi ya kindugu kufanyika.
- Kwa watoto wa umri unaofaa, kuna haja ya kuwapatia uelewa na kuwahamasisha kufahamu umuhimu wa mahusiano na ngono salama, haki ya kusema hapana iwapo huridhii kushiriki mahusiano ya kingono na pia kujikinga dhidi ya VVU/UKIMWI na magonjwa mengine ya zinaa. Mafunzo haya yanatakiwa kutolewa mashuleni na katika vituo vya malezi kwa kutumia wakufunzi waliopata mafunzo hayo.
- Upo pia umuhimu wa kuwahusisha watoto na vijana waishio peke yao mitaani ili watambue madhara ya utumiaji dawa za kulevya.

### Utafiti

- Kuna upungufu katika kufahamu mambo wanayokumbana nayo wasichana wanaoishi peke yao mitaani jambo linaloonyesha umuhimu wa kufanya utafiti utakaolenga maneno na ukweli wa maisha ya wasichana wanaoishi peke yao mitaani nchini Tanzania na Kenya.

### Hitimisho

- Serikali zote mbili za Tanzania na Kenya zimepiga hatua kubwa katika kuboresha maisha ya watoto katika nchi zao. Hata hivyo yapo mengi yanayohitaji kufanywa ili kuhakikisha kuwa watoto na vijana, ambao ni wadau wakubwa kijamii kama watoto na wazazi wa siku zijazo, wanaweza kufikia viwango vyao vya juu katika kujiendeleza na kutoa mchango wao kikamilifu katika uchumi, kulea kizazi kijacho, na kujenga jamii endelevu. Huduma za pamoja zinatakiwa ili kukidhi mahitaji ya watoto wote waishio katika mazingira hatarishi na kuhakikisha kuwa huduma za kurekebisha hali hiyo zinapatikana katika ngazi ya mtu binafsi, familia na jamii ili kutatua masuala ya msingi kama vile umaskini, masuala ya kiafya na upatikanaji wa elimu sambamba na kujihusisha na masuala yanayomgusa mtu binafsi na mazingira ya familia moja moja na watoto. Hili linawezekana tu kwa kufanya kazi kwa ubia na serikali ya kitaifa, mashirika ya kijamii, jamii husika, familia na watoto wenyewe.

Railway Children
1 The Commons
Sandbach
Cheshire
CW11 1EG
UK

+44 (0)1270 757596

Registered Charity Number: 1058991

Railway Children Africa
P.O. Box 138
Mwanza
Tanzania

+255 (0)685 22 74 84

Company No: 77698
NGO compliance No: 1381

www.railwaychildren.org.uk

ISBN Number: 978-0-9563998-3-0

RAILWAY children
Fighting for street children